

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MADAKTARI (NAFASI 164)

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imepata kibali cha ajira ya Madaktari 164 watakaofanya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Hivyo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inapenda kuwatangazia **Madaktari wa Binadamu** na **Madaktari wa Meno** waliohitimu katika vyuo mbalimbali vya elimu ya juu vinavyotambulika na Serikali kuwasilisha maombi ya nafasi za ajira kuanzia **tarehe 22/08/2020** ili kujaza nafasi mbalimbali zilizoainishwa katika Hospitali za Halmashauri na Vituo vya Afya nchini.

Waombaji wawe na Shahada ya Udaktari wa Binadamu/Meno kutoka Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali wawe wamemaliza mafunzo ya kazi kwa vitendo (*Internship*) kwa muda usiopungua mwaka mmoja na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (*Medical Council of Tanganyika*).

SIFA ZA MWOMBAJI;

- i. Awe raia wa Tanzania;
- ii. Awe na umri usiozidi miaka 45;

- iii. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea;
- iv. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali au asiwe Mwajiriwa wa Hospitali za Mashirika ya Dini ambaye mshahara wake unalipwa na Serikali; na
- v. Asiwe amewahi kuajiriwa Serikalini au ana cheki namba.

MAOMBI YOTE YAAMBATISHWE NA NYARAKA ZIFUATAZO:

- (i) Barua ya maombi ya kazi ikieleza vituo vitatu (3) ambavyo mwombaji angependa kupangiwa kufanya kazi.
- (ii) Nakala ya cheti cha kidato cha nne/sita;
- (iii) Nakala za Vyeti vya Taaluma;
- (iv) Nakala ya cheti cha kuzaliwa;
- (v) Nakala ya cheti cha usajili kamili (*Full Registration*) au Leseni ya kufanya kazi ya taaluma husika; na
- (vi) Maelezo binafsi (CV), yakionesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani/namba za simu za kiganjani za wadhamini wasiopungua wawili.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE

- (i) Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi katika vituo walivyoomba;
- (ii) Waombaji waliosoma nje ya nchi wanatakiwa waambatishe *Equivalent Certificate* kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU); na
- (iii) Mara baada ya kupangiwa kituo, hakutakuwa na nafasi ya kubadilishiwa kituo cha kazi.

Orodha ya Hospitali na Vituo vya Afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa vyenye nafasi wazi kwa ajili ya ajira za Madaktari 164 imeambatishwa.

Maombi yote yatumwe kwa njia ya mtandao (*online*) kupitia mfumo wa kielektroniki unaopatikana kupitia anuani ifuatayo: **ajira.tamisemi.go.tz**.

Maombi yoyote yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kuletwa moja kwa moja Ofisini hayatafanyiwa kazi.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 31 Agosti, 2020 saa 9:30 alasiri.

Tangazo hili linapatikana katika tovuti ifuatayo:

www.tamisemi.go.tz

Limetolewa na: Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais - TAMISEMI,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P 1923,
41185 DODOMA.
22 Agosti, 2020